# NIA ZA SALA ZA BABA MTAKATIFU
# ALIZOTOA KWA MTANDAO WAKE WA SALA ULIMWENGUNI
# KWA MWAKA 2027

## JANUARI

### Ili kutambua nguvu ya sala.

Tusali ili kwamba sisi sote katika Kanisa tugundue nguvu ya sala kama makutano binafsi na Bwana, ambayo huleta mabadiliko mioyoni mwetu na ulimwenguni.

## FEBRUARI

### Ili wale wanaowahudumia wengine wapate usaidizi.

Tusali kuwaombea wale wanaotunza afya kamili ya wengine wapate usaidizi wanaohitaji, na wawe na subira, hekima na ujasiri, ili kufungua njia za uponyaji wa ndani na matumaini.

## MACHI

### Ili hadhi ya maisha ya mwanadamu iheshimiwe.

Tusali ili kwamba katika utamaduni unaojikita katika uzalishaji na matokeo ya haraka haraka, tuwe na uwezo wa kugundua na kuthamini hadhi ya kipekee ya kila mtu, yetu wenyewe na ya wengine.

## APRILI

### Kwa ajili ya sanaa kama zawadi inayotunza ubinadamu.

Tusali ili sanaa itambuliwe kama zawadi ya kweli inayotunza ubinadamu wetu, inayotutia moyo na kutusaidia kutafakari uzuri wa Mungu katika uumbaji.

## MEI

### Ili ajili ya fursa za ajira kwa wote.

Tusali ili maendeleo ya kiteknolojia yafungue nafasi za kazi zenye heshima, na ushirikiano kati ya kizazi kimoja na kingine ufanye iwezekane kuwa na mustakabali ambapo kila mtu anaweza kutoa vipaji vyake kwa ajili ya manufaa ya wote.

## JUNI

### Kwa ajili ya matumizi bora ya akili bandia.

Tusali ili maendeleo ya akili bandia yawe daima kwa ajili ya kuhudumia hadhi ya binadamu, na tujue kuitumia kwa hekima.

## JULAI

### Kwa ajili ya mababu na wazee

Tusali ili sisi waumini wa Kanisa tuthamini hazina ya imani na hekima wanayotupatia babu na wazee, tukiwa tayari kujifunza kutokana na waliyopitia.

## AGOSTI

### Kwa ajili ya wito wa vijana.

Tuombe ili vijana wanaotafuta wito wao wa maisha watambue katika Yesu Kristo rafiki anayeambatana nao katika safari ya maisha na wanaweza kumfunulia mioyo yao.

## SEPTEMBA

### Kwa ajili ya wongofu wa kina wa kiikolojia.

Tuombe ili tuweze kujifunza kuishi katika uhusiano mpya na uumbaji, tukiuulinda kwa haki, na katika kutafakari uumbaji, tupate njia ya kuelekea maisha yenye uwiano na kukidhi zaidi.

## OKTOBA

### Kwa ajili ya jumuiya za Kikristo.

Tuombe ili kila parokia, jumuiya au kikundi cha Kikristo kiwe kituo panaponzia kazi za kimisionari, mahali wanapolelewa mitume wapya kwa huduma ya Injili.

## NOVEMBA

### Kwa ajili ya mapokezi ya wahamiaji.

Tusali ili, kwa mastahili na faraja ya Familia Takatifu ambayo ilipitia machungu ya kung'olewa kutoka kwao, wahamiaji na wakimbizi wapete jumuiya zinazowakaribisha kwa hadhi, mshikamano na kuwajumuisha kweli katika maisha.

## DESEMBA

### Kwa ajili ya wito wa familia ya Kikristo.

Tusali ili familia za Kikristo ziwe mashahidi hai wa Injili katika jamii, zikijifunza zaidi na zaidi kuwa nyumba ambamo imani, matumaini na mapendo vinakuzwa.